Mafunzo kwa Kamati ya Kitaalamu ya Wilaya (DDTC)

# Taratibu za maombi ya kibali cha kufungua duka la dawa muhimu

imetayarishwa na TFDA/MSH

# utangulizi

- Kanuni za Maduka ya Dawa Muhimu zinatoa madaraka kwa ngazi ya kijiji, kata, wilaya na Taifa katika kushughulikia maombi ya vibali vya Duka la Dawa Muhimu
- Mkaguzi anapaswa kujua taratibu za ufunguaji wa maduka ya aina hii ili kudhibiti maduka ambayo yanaweza kufunguliwa bila kukamilisha taratibu hizo.

# Fomu za Maombi

- Fomu za maombi ya kuanzisha duka la dawa muhimu (DLDM) zinapatikana kwa Katibu wa DDTC ambaye ni mfamasia wa wilaya
- Gharama ya fomu ni 2,000/=
- Wanaotaka kufungua Duka la Dawa Muhimu katika vijiji, watawasilisha fomu hizi kwa Afisa Mtendaji wa Serikali ya Kijiji (VEO).
- Wanaotaka kufungua Duka la Dawa Muhimu (ADDO) katika miji midogo, watawasirisha fomu hizi kwa Afisa Mtendaji wa Kata (WEO).

# Majukumu na Wajibu wa serikali ya kijiji

Serikali ya kijiji ina jukumu la kumhoji mwombaji kuhusu:

- Umuhimu wa huduma hiyo katika sehemu yao
- Tabia ya mwombaji na uhusiano wake na jamii
- Uraia wake
- Anwani ya sehemu anayoishi
- Biashara anazofanya au alizowahi kufanya hapo zamani
- Kupata taarifa zaidi kutoka kwa mwombaji kuhusu sehemu anapotaka kufungua Duka la Dawa Muhimu

# Majukumu na Wajibu wa Kata

- Kamati ndogo ya Afya ya kata itapokea maombi toka ngazi ya kijiji, kufanya ukaguzi wa awali na kuwasilisha taarifa kwa WDC kwa uamuzi kabla ya kuzipeleka kwa DDTC
- Ngazi ya kata ina majukumu yafuatayo:
  - Kupitia fomu za maombi ya DLDM
  - Kumhoji mwombaji pamoja na Watoa Dawa watarajiwa

# Majukumu ngazi ya kata ……

- Kufanya ukaguzi wa awali wa jengo na mazingira yanayozunguka jengo
- Kuwasilisha ripoti ya ukaguzi wa jengo katika Kamati ya Kitaalam ya Dawa ya wilaya.
- Kuzishauri ngazi za juu kuhusu namna bora ya kuendesha DLDM

# Kamati ya Kitaalamu ya Wilaya

- Kupitia maoni na mapendekezo ya maombi ya kuanzisha DLDM kutoka WDC
- Kupokea ripoti za ukaguzi kutoka ngazi ya Kata na kuzitolea maamuzi
- Kukagua sehemu zote zinazoshughulika au kutoa huduma za dawa katika Wilaya kupitia timu ya wakaguzi
- Kukubali au kukataa maombi ya DLDM kwa niaba ya TFDA

# Kamati ya Kitaalamu ya Wilaya…

- kuwasilisha kwa Mamlaka orodha ya waombaji waliokubaliwa na nakala yake kuwasilishwa kwa kamati ya kitaalam ya dawa ya mkoa (RDTC)
- Kupitia kwa katibu wa kamati, kuwaarifu waombaji wote kuhusu maamuzi yaliyotolewa na Kamati

# Kusajiliwa kwa Duka la Dawa Muhimu (ADDO)

- Baada ya DDTC kupitisha maombi, mwombaji aliyekubaliwa atapata kibali cha DLDM (accreditation certificate)
- Kuna malipo ya ada ya mwaka. (80% inabaki kwa DDTC)
- Kibali kitarumruhusu mwombaji kupewa leseni ya biashara ya Duka la Dawa Muhimu
- Kibali kinaisha muda ifikapo 30 Juni

# Mojawapo ya duka la Dawa Muhimu Tunduru, Ruvuma



# Mambo ya kuzingatia

- Kibali kinatolewa kwa jengo husika, hivyo hakiwezi hamishwa kwenda duka jingine
- Jengo lazima liwe na vyumba viwili (cha kutolea dawa na stoo)
- Umbali kati ya duka na duka na idadi ya watu izingatiwe
- Duka lazima liendeshwe na mtoa dawa aliyeidhinishwa na TFDA
- Duka liuze dawa zilizoruhusiwa tu !!
- Duka linapofungwa lazima taarifa itolewe kwa DDTC na kibali kirudishwe